

Tunafurahia hali ya hewa na hali ya maisha nzuri katika Queensland. Hata hivyo, hatari za kimaumbile kama vile tufani, dhoruba na mafuriko ni sehemu tusioepukika ya mazingira yetu. Historia imeonyesha kwamba hatuwezi kunyamaza hivyo tu kuhusu hatari ambazo zinaletwa na haya.

Chukua muda kujitayarisha dharura kwa:

- Kutayarisha Mpango wako wa Dharura;
- Kutayarisha Mkoba wako wa Dharura,
- Kutayarisha nyumbani pako; na
- Sikiliza onyo zinazotolewa

Hatua hizi rahisi zinaweza kusaidia katika kujitayarisha, kuokoka, na hata kupunguza athari ya majanga ya kimaumbile.

Vifuatavyo ni anuwai ya vidokezo vilivyopendekezwa vya kukusaidia kujitayarisha na Mkebe wako wa Dharura na kuhakikisha kwamba kila mtu katika familia yako amejitayarisha:

- Hifadhi Mkebe wako wa Dharura mahali pa salama, panapofikika.
- Hakikisha wanafamilia wote wanajua mahali pa Mkebe wako wa Dharura.
- Weka nakala ya Orodha hii ya Mkebe wa Dharura katika mkebe wako.
- Angalia yaliyomo katika mkebe wako mara kwa mara kuhakikisha kwamba vitu vyote vinafanya kazi na havijachina.
- Zungumzia yaliyomo kwenye mkoba pamoja na familia yako na uhakikishe kwamba kila mmoja anajua cha kufanya pindi dharura itakapotokea.

Orodha zifuatazo zinajumulisha vitu vya kuwa navyo katika mkoba wako siku zote na vingine vya ziada vinavyohitajika kuongeza kwenye mkebe wako wakati wa misimu ya dhoruba na tufani wakati ambapo onyo za hali ya hewa zinapotolewa.

Vitu hivi vya kujumuishwa katika Mkebe wako Dharura siku zote

Chakula na maji

Mseto wa vyakula viso-haribika

Maji ya chupa

Vitu vya kimatibabu na usafi

Mkebe wa Huduma ya Kwanza na kitabu chake cha mwongozo

Dawa muhimu, zilizoshauriwa na kipimo husika

Shashi

Mswaki/dawa ya meno

Sabuni/shampuu

Vitu vya usafi wa kibinafsi

Mwangaza

Kurunzi/tochi na iliyo na betri za ziada

Taa inayotumia betri kuwaka

Mawasiliano

Redio inayotumia betri pamoja na betri za ziada

Simu ya kienyeji ya waya

Kadi ya simu iliyo na hela za kupigia pamoja na sarafu za kupiga simu

Mavazi na viatu

Sweta nzito, koti lisiloingiza maji, kofia na glovu za kila mtu

Viatu vya kufunika vidole vya miguu au buti kwa kila mmoja

Zana na nyenzo

Firimbi, kisu cha kazi, kichirizi/tepu ya masking

Mikoba ya kutupa taka ya plastiki, vifungo

Miwani ya Usalama na miwani ya jua

Vitu vya ziada

Vitu Maalum kwa Watoto wachanga (nepi, fomula nk)

Vitu maalum vinavyohitajika na watu wakongwe au watu walio na mahitaji maalum

Funguo za ziada za nyumba na gari

Chakula cha wanyama wapenzi, maji na mahitaji mengine ya wanyama

Nyaraka muhimu

Weka nakala halisi au idhinishwa za nyaraka zifuatazo katika Mkoba wako Dharura. Skani nakala ya nyaraka hizi na uzihifadhi katika diski mwake ya USB au CD naujumishe kwenye mkoba wako. Weka vitu hivi vyote katika mabegi ya plastiki yaliyofunikwa.

Karatasi za bima za nyumba na yaliyomo, magari, na vitu vyenye thamani

Orodha ya bidhaa muhimu za familia

Nyaraka za wosia na za bima za maisha

Nyaraka za hati za umiliki wa nyumba/rehani

Vyeti vya kuzaliwa na ndoa

Pasipoti/ maelezo ya visa

Hisa na bondi

Kadi za utozaji wa kimatibabu, malipo ya pensheni, kumbukumbu ya chanjo

Maelezo ya akaunti ya benki na kadi ya mkopo

Nakala chelezo ya faili muhimu za tarakilishi

Mpango wa Dharura wa familia ulio na nambari za simu za mawasiliano za dharura.

Vitu vingine vya dharura vya kutayarisha nyumbani:



Mkoba wa zana



Nyenzo za ziada



Jiko la kubebeka au la gesi

siku zote kumbuka

Kuwa na Mkoba wa Dharura ni hatua muhimu kwa familia yako kujitayarisha, kuokoka na kuweza kudhibiti dharura zinazowapata. Wanafamilia wote wanahitaji kujua kwamba Mkoba wako wa Dharura umewekwa wapi. Angalia na usasishe yaliyomo katika Mkoba wa Dharura mara kwa mara.

Mkoba wa Dharura



Vitu vya ziada vya kujumuisha katika Mkoba wako wa Dharura wakati msimu wa tufani na dhoruba.

Onyo za hali ya hewa zinatolewa wakati wa dharura kama vile mafuriko, dhoruba na tufani zinatarijiwa. Wakati wa msimu wa dhoruba na tufani ongezea vitu vifuatavyo katika Mkoba wako wa Dharura.

Inapendelewa kuweka akiba ya vitu hivi katika mkoba wako kila wakati. Hata hivyo, kama huna nafasi ya kutosha katika mkoba wako—weka maelezo ya ni wapi pa kupata vitu hivyo vya ziada katika nyumba yako ili uweze kuvichukua haraka. Kama unao wageni wakati wa dharura, utahitaji vitu vyao vilevile pia.

Chakula na maji

katika mkoba au Mahali

Vitu vya siku tatu vya chakula kiso-haribika (pamoja na

Kifunguo kopo, zana za upishi, sahani na vyombo)

Maji safi katika mikebe iliyofungwa

(lita 10 kwa kila mtu zinapendekezwa kwa matumizi ya siku tatu)

Tembe za kusafisha maji

Vifaa vya kimatibabu na usafi

Vifaa vya ziada vya kimatibabu

Vifaa vya ziada vya kujikwatua na vifaa vya usafi, skrini ya kuzuia jua na

Kinga wadudu

Maelezo ya ushauri wa dawa zote

Miwani ya ziada

Zana, vitu vya mawasiliano na akiba ya vitu

Tepu za masking pana kwa kutumia madirishani

Spana au koleo za kuzima huduma zote

Hema au turupali

Blanketi za safu na za joto

Simu ya mkono, betri ya ziada na chaja

Mavazi na viatu

katika mkoba au vinavyopatikana

Badilisha nguo za kila mmoja, zinazohifadhiwa katika mabegi ya plastiki

Nguo za ziada na matandiko

Vitu vya ziada

Vitu vya ziada kwa watoto wachanga (fomula ya ziada, nepi nk)

Vitu vya ziada kwa watu wakongwe au watu wenye mahitaji maalum

Pesa za ziada endapo wahudumu wa benki wa elektroniki hawataweza kufanya kazi

Wanyama wapenzi- vitu na taarifa kuwahusu, (mf karatasi za daktari wa wanyama, ukanda,

chakula & maji, utambulisho wa jina kwenye ukosi, vitanda vya wanyama wapenzi,

sufuria ya choo & skupa, hamali au sindano, dawa)

Wakati wa dharura, huenda kukawa na hitilafu za umeme na maji.


Hakikisha ya kwamba una vitu vifuatavyo kwa utoshelevu wavyo:

Jiko la makaa au la kubebeka na mafuta au makaa

Betri zilizochajiwa kamilifu na simu ya mkononi

Betri za ziada za kurunzi na redio

Esky au jokofu linaloendeshwa kwa gesi au betri



Broshua hii ni ya taarifa tu na imetolewa kwa roho safi. Idara ya Usalama wa Jumuia, Usimamizi wa Dharura wa Queensland na Huduma ya Dharura ya Serikali yote haitawajibikia mtu yeyote kwa mujibu wa kupoteza au kuharibika kokote (kukiwemo athari ya kupoteza au kuharibu) ambayo kunaweza kupatikana au kutozwa, au kunakoweza kutokea moja kwa moja au vinginevyo, kwa mujibu wa kutegemea wa mtu yeyote katika taarifa ilimo kwenye broshua hii.

Kwa taarifa zaidi kuhusu kujitayarisha kwa dharura tembelea www.disaster.qld.gov.au

ukurasa 2 wa 2 Swahili